

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtentaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inatarajia kupokea Mwenge wa uhuru tarehe 13 juni, 2018. Mwenge wa uhuru ukiwa Masasi utakimbizwa kwenye vijiji 18 kata 8 na tarafa 3 na utapokelewa katika kijiji cha Mpeta na kukimbizwa katika Vijiji vya Chiungutwa, Ndwika, Nagaga, Namombwe, Mkwaya na utakesha katika kijiji cha Mnavira kata ya Mnavira.

Mwenge wa Uhuru ukiwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi utaweka mawe ya msingi katika miradi minne (4) , kuzindua klabu ya wapinga rushwa na kugawa hundi za mikopo kwa vikundi 41 vya wanawake na vijana zenyen thamaani ya shilingi milioni 144,219,000. Hivyo miradi yote itakayopitiwa na mwenge wa uhuru kwa mwaka 2018 ina thamani ya shilingi bilioni 2,385,219,000

Miradi itayowekewa mawe ya masingi na Mwenge wa Uhuru ni mradi wa ujenzi wa madarasa 7, maabara 1 mabweni 2 na jengo la utawala 1 katika shule ya wasichana ndwika unaoghalimu shilingi milioni 400, ujenzi wa majengo ya wodi 1, chumba cha upasuaji 1,maabara 1, mochwari 1 na nyumba ya mtumishi 1 katika kituo cha Nagaga unaogharimu shilingi 400, mradi wa maji makong'onda -rivango unaogharimu shilingi bilioni 1,415,000,000, ujenzi wa madarasa 3 shule ya msingi Mnavira unaogharimu shilingi milioni 26,000,000 kwa nguvu ya wananchi na halmashauri na hundi za mikopo kwa vikundi 41 vya wanawake na vijana zenyen thamani ya shilingi milioni 144,219,000

Hivyo wananchi wote mnakaribishwa kuupokea na kuushangilia Mwenge wa Uhuru utakapofika katika halmashauri yetu kwani mwenge unadumisha Amani na Umoja. Ujumbe na Kauli mbiu ya Mbio Za Mwenge wa Uhuru 2018 ni “UWEKEZAJI ATIKA ELIMU” chini ya kauli mbiu inayosema “ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA, WEKEZA SASA”

Imetolewa na

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI**